TANGAZO LA SERIKALI NA. 871 la tarehe 1/12 2023

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,

(SURA YA 147)

## AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128 (2))*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI NA WIZARA YA AFYA, 2023.

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye gari moja litakalotumika na Wizara ya Afya katika mradi wa kutokomeza Malaria, 2023 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika kuanzia tarehe 03 Novemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa gari liloanishwa katika Jedwali la Amri hii lililoingizwa ndani ya nchi au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha litatumika na Wizara ya Afya kwa ajili ya mradi unajihusisha na kutokomeza Malaria unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa gari tajwa litatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itakoma kutumika tarehe 1 Mei, 2024

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya injini |
|---|---|---|---|
| 1 | TOYOTA LANDCRUISER HARDTOP 10-SEATER, 5 DOORS | JTEEB71J30-F024866 | 1HZ-1040696 |

Dodoma,
21 Novemba, 2023.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*